# KENYA EDUCATORS CONSULTANCY EXAMS
# ENGLISH READING ACTIVITIES
# TERM 2 2023

## KISWAHILI SEC. A ACTIVITIES ASSESSMENT

NAME____________________________DATE ________ ____

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Nilikuwa gredi ya tano kipindi hicho, nilikuwa mimi na wadogo zangu wawili. Kawaida yetu ilikuwa kila tukimaliza kula chakula cha usiku tunapumzika kidogo, halafu tunasali, na kama kuna mwenye homework anafanya na anaingia kitandani na kulala. Siku hiyo baba alikuwa hajarudi kipindi nafanya homework baada ya kuwa tumemaliza kusali na mama pamoja na wadogo zangu walikuwa tayari wamesha lala. Takribani saa sita usiku baba akarudi akiwa chakali amelewa, alibisha hodi mama akaamka na kumfungulia, alikuwa mkali sijawahi kumwona baba yangu akiwa mkali vile, akamnasa mama makofi mbele yangu, mama aliumia kwa maumivu, hali ile iliniuma sana mpaka nikalia. Hakuishia hapo bali alimrushia mateke kana kwamba anapigana na mwanaume mwenzake.

A. Msimulizi alikuwa gredi ya ngapi?
B. Baada ya kula chakula cha usiku walikuwa wakifanya nini?
C. Baba alimfanyia nini baada ya kurudi nyumbani?

# KISWAHILI SEC. A ACTIVITIES ASSESSMENT

NAME______________________________________ DATE

________ ________

## Kusoma Kwa Sauti

Mfalme Mbezi alipoona kuwa walinzi wake hawarudi katika siku ile ile aliyo wapangia, akaamua aongeze siku moja zaidi kuwasubiria na kama hawatafika aweze kufanya kitu ili kuhakikisha kuwa lulu ya binti yake inapatikana kwahali yoyote ile. Ilipofikia majira ya saakenda mfalme Mbezi alihisi kuwa huenda watuwake waliokuwa wamekwenda kisiwa cha mikwingwina wamep-atwa na mabaya. Akawaambia watuwake waliokuwa pamoja nae kuwa, "Lulu kwaajili ya binti yangu nilazima ipatikane na sipo tayari kurudi Mgombezi bila lulu" Akawaambia watu wake kuwa hakuna mtu atakayebakia ng'ambo yakisiwa cha Mikwingwina

**Compiled and Distributed by Kenya Educators Consultancy, P.O.BOX 15400-00500, Nairobi.Tel 0724333200 E-mail kenyaeducators@gmail.com. ORDER MARKING SCHEMES ATwww.kenyaeducators.co.ke or Contact 0724333200/0768321553/079549118**5